

Unachotarajia: Maelezo kuhusu Kutembelea Kituo cha COVID-19 Kinachopima Sampuli ya Mate

Unachotarajia ukitembelea kituo cha COVID-19 kinachopima sampuli ya mate.

Kwanza, hakikisha hujavuta sigara, hujakula, kunywa au kutafuna chochote dakika 30 kabla ya kuwasilisha sampuli yako ya mate.

Usinywe hata maji.

Njoo na simu ya kisasa yako, kadi ya bima na anwani ya barua pepe inayotumika ukiwa unayo.

Ikiwa huna simu ya kisasa, zipo kompyuta kibao zilizoeliwa kituoni ambazo unaweza kutumia.

Ikiwa huna bima, bado unaweza kupimwa bila malipo.

Hutapewa bili.

Na ikiwa huna anwani ya barua pepe inayotumika, wafanyakazi wanaweza kutumia nambari ya simu kukupigia na kukupa matokeo yako kwa njia ya simu.

Unahimizwa uandikishe miadi utakayohudhuria, lakini wageni wanaokuja bila miadi pia wanakaribishwa.

Ukifika, fuata maagizo yaliyo kwenye ishara ili ujiandikishe au kuingia kwenye miadi yako.

Wafanyakazi watakuomba ubadilishe barakoa yako uvae barakoa mpya ya kimatibabu.

Hatua hii husaidia kudumisha usafi wa hali ya juu iwezekanavyo.

Wafanyakazi watakuuliza kama unahitaji mkalimani na ikiwa una simu ya kisasa.

Kisha watakupa kisanduku na kukupeleka kwenye meza.

Utatumia simu yako ya kisasa kuchanganua msimbo wa QR ulio kwenye meza.

Hatua hii itakupeleka kwenye tovuti ya kufanyia vipimo ambapo unaweza kujaza maelezo yako.

Ikiwa una maswali yoyote, wafanyakazi wako tayari kukusaidia.

Baada ya kujaza maelezo yako, tovuti itakuongoza kwenye kila hatua ya kupima sampuli ya mate.

Utahitaji kuweka mate ya kutosha yajaze kiasi kinachopita mstari.

Mapovu hayatazingatiwa.

UNACHOTARAJIA: MAELEZO KUHUSU KUTEMBELEA KITUO CHA COVID-19 KINACHOPIMA
SAMPULI YA MATE

Ukigonga chupa utaondoa mapovu ili uweze kuona kiasi kilichosalia kujazwa.

Chupa yako ikijaa hadi kwenye laini, ondoa faneli ya kuchukua mate kisha ufunge kifuniko kwa vihifadhi vya samawati.

Endelea kufunga kifuniko hadi kigawanyishaji kilicho kati ya kihifadhi cha samawati na sampuli yako ya mate kipasuke hivi kwamba unaweza kutingisha chupa ili kuchanganya kihifadhi cha samawati na mate.

Tingisha chupa kwa sekunde 5.

Mwishowe, peleka chupa yako kwenye meza ya kuwasilisha sampuli na utupe vifurushi vya kisanduku cha kupima.

Utatumiwa matokeo yako kwa barua pepe ndani ya saa 48.

Au ikiwa huna barua pepe, utapigiwa simu kwa nambari ya simu uliyopeana.

Ikiwa una maswali yoyote kuhusu mchakato wa kuchukua sampuli, waulize wafanyakazi walio kwenye kituo cha kupima sampuli ya mate.

Asante kwa kupimwa na kusaidia kulinda usalama wa jamii zetu!

Minnesota Department of Health
Communications Office
PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-4989
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

9/11/20 (Kiswahili/Swahili)

Ili upate maelezo haya kwa muundo tofauti, piga simu: 651-201-4989